



## WasifuwaMstahili-heshima Sista Maria Carola

Fiorina Cecchin alizaliwa mjini Cittadella tarehe 3 Aprili 1877. Akiwa na umri wa miaka 19 aliingia katika Chumba Kidogo cha Mungu Mpaji, "Cottolengo" huko Torino. Alitwaa vazi la kitawa na akaanza malezi ya noviziati tarehe Oktoba 1897, akichukua jina la Sista Maria Carola.

Mwaka 1899 aliweka nadhili za utawa. Alitoa huduma kwanza jikoni katika Chuo cha Giaveno, na kisha katika jiko kuu la Chumba Kidogo. Wito wake ulikuwa majitoleo, kumpenda Mungu na mioyo ya watu.

Mnamo Januari 28, 1905, aliondoka kuelekea Afrika. "Kituo" chake cha kwanza kilikuwa Limuru, kisha Tuthu, Iciagaki, Mugoiri, Wambogo, na mwishowe Tigania-Meru. Alionekeana kuwa mwanamke mwenye busara na hekima, mtendaji na mchaji. "*Na bôna mort a pagrà tut*", kifo chema kitalipa kila kitu, huu ulikuwa ndio usemi wake wa kawaida. Yote kwa ajili ya Mbinguni!

Pale Iciagaki nyumba ilikuwa kama mahame, karai moja ilitumika kama sufuria, hivyo Sista Carola kama mkuu wa nyumba aliyarekebisha mazingira pawe pazuri pa kuishi. Alilima bustani ya mbogamboga, alipamba uani na kukusanya pamoja jumuiya ndogo chini yake, akiongozwa na upendo usio na kipimo wa Yesu.

Wakati inaonekana kwake mwanzo wa maisha ya kawaida ya umisionari, "utii" unamfikia kuondoka kwenda Mugoiri, kisha kwenda Wambogo kuchukua nafasi ya masista wawili walioenda kuhudumu katika hospitali ya muda. Ni wakati wa kutisha wa vita vya mwaka 1915-1918 kipindi alichishi kwa mwanga na nguvu ya "*Caritas Christi urget nos!*", kama Cottolengo. Shuhuda asiyechoka wa upendo wa Mungu Baba kwa walio maskini zaidi, majitoleo, pamoja na huduma za dharura zaidi, upendo mkuu: tangazo la Yesu, Mkombozi pekee wa mwanadamu. Kituo chake cha mwisho kilikuwa Tigania, ambapo kati ya matatizo anapenda kuimba "*na bôna mort*". Inaonekana ajabu leo, lakini ni watakatifu, mashujaa na mashahidi wangapi katika Kanisa waliotokana na tafakuri ya mambo ya mwisho! Ilikuwa hivyo kwa Sista Maria Carola ambaye ni wa mwisho kuondoka Afrika Oktoba 25, 1925. Alipokuwa njiani kurudi kwa meli, mnamo Novemba 13, 1925 alikwenda kukutana na Mungu. Baada ya kuhadhimisha mazishi ndani ya meli, mwili wake ulizikwa katika mawimbi ya Bahari ya Shamu. Hakupewa nafasi ya kufurahia paradisi katika Chumba Kidogo. Yesu alimtaka moja kwa moja katika Paradisi ya kweli. Hata leo anabaki kuwa mfano wa maisha ya umisionari, utakatifu na kujitolea kishujaa kwa Kristo na kwa mioyo inayohitaji kuokolewa!

Mnamo 23 Novemba 2020, Baba Mtakatifu aliidhinisha kuchapishwa kwa tangazo rasmi kuhusu fadhila zake za kishujaa, hatua moja karibu na kutangazwa mwenyeheri.

**Suor Lucia Mossucca - Stefano Di Lullo**

[www.cottolengo.org](http://www.cottolengo.org)

Via Cottolengo, 12 - 10152 Torino, cell. +39 345 6216561

[ufficiostampacottolengo@cottolengo.org](mailto:ufficiostampacottolengo@cottolengo.org)